**HOTUBA YA MHE. PROF. MAKAME M. MBARAWA (MB), KATIKA HAFLA YA KUSAINI MKATABA WA UKAMILISHAJI WA MRADI WA UJENZI WA JENGO LA ABIRIA KATIKA KIWANJA CHA NDEGE CHA MWANZA, TAREHE 28 MACHI, 2024.**

Mheshimiwa Amos Makalla, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza,

Ndg. Michael Lushinge Masanja, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mwanza,

Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge za Miundombinu, Uwekezaji wa Mitaji ya Umma na Hesabu za Serikali,

Makatibu Wakuu na Naibu Katibu Mkuu,

Ndg. Juma Hassan Fimbo, Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Wizara ya TAA,

Ndg. Mussa Mbura, Mkurugenzi Mkuu TAA

Ndg.Balandya Elikana, Katibu Tawala Mkoa wa Mwanza,

Waheshimiwa Wabunge wa Majimbo ya Ilemela, Nyamagana, Kahama na Geita,

Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya za Ilemela na Nyamagana,

Wakurugenzi Manispaa ya Ilemela na Halmashauri ya Jiji la Mwanza,

Menejimenti ya TAA,

Wadau wa Sekta ya Usafiri wa Anga,

Waandishi wa Habari,

Ndugu Wageni Waalikwa,

Mabibi na Mabwana,

Itifaki imezingatiwa.

***Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano waTanzania!***

***Ndugu Wageni Waalikwa,***

Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia siku ya leo kuweza kushuhudia utiaji saini mkataba wa mradi wa ukamilishaji wa jengo la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Mwanza.

***Ndugu Wageni Waalikwa,***

Kama mnavyofahamu, Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan** imeendelea kufanyia kazi ahadi za Chama cha Mapinduzi zilizo katika Ilani ya Uchaguzi kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo miradi ya ujenzi na uendelezaji wa viwanja vya ndege hapa nchini.

***Ndugu Wageni Waalikwa,***

Wananchi wa Mkoa wa Mwanza na Kanda ya Ziwa, tuna kila sababu ya kujivunia utekelezaji madhubuti wa ahadi za Chama chetu cha Mapinduzi na namna zilivyokuza uchumi, biashara, pato la taifa na kupelekea kuboreka kwa huduma kwa wananchi. Sisi sote ni mashahidi wa uwekezaji na uboreshaji wa bandari zetu; ujenzi wa meli mpya ya MV Mwanza ambayo tayari imeingia wiki hii majini kwa majaribio; na Ujenzi wa reli ya mwendo kasi (SGR) inayotarajia kukamilika kipande cha Isaka-Mwanza ifikapo mwishoni mwa mwaka 2025.

***Ndugu Wageni Waalikwa,***

Kupitia Wizara ya Uchukuzi, tumeshuhudia pia kuendelea kutekelezwa kwa miradi mingine ikiwemo ujenzi wa Kiwanja kipya cha Kimataifa cha Msalato, ukarabati wa viwanja vilivyopo; pamoja na ununuzi wa ndege mpya za abiria na mizigo. Mtakumbuka, juzi tumeshuhudia mapokezi ya ndege mpya aina ya Boeing 737-9MAX ambayo imefanya ndege zilizonunuliwa kufikia 15 mpaka sasa.

***Ndugu Wageni Waalikwa,***

Napenda kutumia nafasi hii kwa niaba ya Wizara ya Uchukuzi na wadau wa usafiri na usafirishaji kumshukuru **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuridhia na kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hii anuai. Leo hii tumeshuhudia kusainiwa kwa Mkataba wa ukamilishaji wa Mradi wa ujenzi wa jengo la abiria katika kiwanja hiki cha Mwanza.

***Ndugu Wageni Waalikwa,***

Kama ilivyoelezwa na Mkurugenzi Mkuu katika taarifa yake; Fedha za utekelezaji wa mradi huu zipo na utatekelezwa na mkandarasi mzawa wa daraja la kwanza, ambaye tunaona tayari yuko eneo la mradi na ameanza maandalizi ya awali. Kupitia mradi huu, ni dhahiri kuwa wananchi wa maeneo ya jirani na mradi watapata fursa za ajira na biashara. Aidha, mkandarasi na wataalamu waliopata fursa ya kutekeza mradi huu wataongeza uwezo wao wa utekelezaji wa miradi na kuwafanya kuwa shindani katika soko la ndani na nje ya nchi.

***Ndugu Wageni Waalikwa,***

Nipende kuwahakikishia kuwa, sina mashaka na uwezo wa TAA katika kutekeleza miradi ya viwanja vya ndege. Ni imani yangu kuwa, TAA itasimamia mradi huu kwa weledi na kuhakikisha kuwa unakamilika ndani ya muda uliopangwa. Kwa hakika kukamilika kwa mradi huu kutawezesha watalii kuweza kuvifikia kwa urahisi vivutio vya utalii vya Serengeti, Rubondo, Sanane, Burigi na kwingineko. Hivyo kuwavutia watalii wengi zaidi kuja nchini na kuimarisha shughuli za kitalii katika maeneo haya.

***Ndugu Wageni Waalikwa,***

Kwa kuzingatia umuhimu wa kiwanja hiki katika kuwezesha usafiri na usafirishaji wa abiria na mizigo katika Ukanda huu wa Ziwa Victoria, ninawaagiza TAA na Mamlaka zinazohusika kuhakikisha Kiwanja cha Ndege cha Mwanza kinakuwa na hadhi ya Kiwanja cha Kimataifa ifikapo Septemba, 2025.

Aidha, Kwa kuwa Serikali imekuwa ikitenga na kutumia fedha nyingi katika kujenga na kuboresha miundombinu ya viwanja vya ndege, ninaielekeza TAA ihakikishe inasimamia na kufanya ukarabati na maboresho ya mara kwa mara ya miundombinu ya viwanja vya ndege. Hii itaifanya miundombinu hii kubaki katika ubora unaotakiwa na kuweza kutumika kwa muda mrefu zaidi.

***Ndugu Wageni Waalikwa,***

Nipende kumalizia kwa kusema kwamba: uendeshaji wa viwanja vya ndege ni zaidi ya utoaji wa huduma ya usafiri kwa abiria na mizigo. Kwa sasa, ulimwenguni viwanja vya ndege vinatumika kibiashara na vimekuwa vikichangia katika uzalishaji wa fursa za ajira, vikijiendesha pasipo kutegemea ruzuku ya Serikali, vikizalisha mapato na kuvutia wawekezaji na watalii. Hivyo, ninawaelekeza TAA kubuni mikakati ya uendeshaji wa viwanja vya ndege kibiashara.

Katika kutekeleza hili, na kwa kuwa taratibu zinaruhusu, TAA washirikiane na sekta za umma na binafsi katika kufanya uwekezaji na uendelezaji wa hoteli za kisasa, kumbi za mikutano na maduka ya kisasa katika viwanja vyetu vya ndege. Ninafahamu mnaendelea na mazungumzo na mwekezaji ambaye anataka kuweka *hub* au kituo maalum cha kuzalisha na kusafirisha bidhaa zake kwenda nje ya nchi kupitia kiwanja hiki. Tafadhali hakikisheni uwekezaji huo unakamilika katika muda ili kuongeza wigo wa mapato kwa wananchi wetu na kwa Serikali.

***Ndugu Wageni Waalikwa,***

Nawashukuru kwa kunisikiliza na nawatakia utekelezaji mwema wa majukumu yenu.

***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!***